# Kusimamia Maliasili

## Wananchi wanasemaje?








## 1. Utangulizi

Katika siku za karibuni, akiba ya gesi asilia imegundulika nchini Tanzania. Serikali ya Tanzania, ikisaidiwa na washirika wa maendeleo, inajaribu kuanzisha hatua sahihi ili kupunguza changamoto zilivyokumba nchi nyingine zikiwemo Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Nigeria na Sudan zikiwemo migogoro ya wenyewe kwa wenyewe, matumizi mabaya ya rasilimali ili kupata faida za kiuchumi zisizonufaisha jamii na upungufu wa uwajibikaji wa serikali.

Mwezi Oktoba 2013 Wizara ya Nishati na Madini ilitoa Sera ya Taifa ya gesi asilia. Sera ilisisitiza jukumu la mashirika yasiyo ya serikali, vyombo vya habari pamoja na jamii kwa ujumla, kuwa ya kuanzisha mazungumzo, ufuatiliaji, kubadilishana taarifa na kukuza "uelewa wa wananchi, uwazi na uwajibikaji." Katika sera hii, Wizara ilizitaja changamoto kadhaa kuhusiana na maendeleo ya sekta ya gesi asilia, ikiwa ni pamoja na: kuweka mfumo wa kisheria; upatikanaji wa rasilimali watu wa kutosha, maarifa na miundombinu; kusimamia masoko ya ndani na nje ya nchi; usimamizi wa mapato; kulinda afya, usalama na mazingira.

Msisitizo katika Sera kuhusu taarifa kwa umma, mazungumzo na kubadilishana mawazo kuna jaza pengo kubwa sana. Kipindi cha miaka michache iliyopita, nchi imeshuhudia mijadala ya umma kuhusu kugawana faida hasa inayokwenda kwa wajasiriamali na wananchi wa Tanzania ikianzishwa. Wawekezaji wa ndani wanadai fursa katika sekta hiyo. Wananchi, hasa kutoka mikoa inayozalisha gesi ikiwemo Mtwara, pia wangependa kupewa sehemu ya faida hizo.

Muhtasari huu umeandikwa na Isis Gaddis na Jacques Morisset (wote wanatoka Benki ya Dunia), na Youdi Schipper na Elvis Mushi (Twaweza). Umeandaliwa na Twaweza, iliyoko Hivos Tanzania. Umetolewa Juni 2014

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301 | barua pepe: uwazi@twaweza.org
www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi

Ni wachache wanaoweza kusema hakuna haja ya watunga sera kusikiliza maoni ya watu juu ya usimamizi wa maliasili. Somo muhimu ambalo tunaweza kujifunza kutokana na uzoefu wa kimataifa usiohesabika wa usimamiaji mbaya, ni hitaji la kuwashirikisha wananchi katika michakato ya kufanya maamuzi. Hii inaweza kusaidia kuziba pengo kati ya matarajio na hali halisi, ambayo inaweza kupunguza uwezekano wa migogoro kutokea. Lakini la muhimu ni kuwa; ni kitu gani Watanzania wangependa au kutarajia kutokana na ugunduzi mkubwa wa maliasili?

Kusaidia kuelewa vyema matarajio ya wananchi, matumaini na wasiwasi uliopo kuhusiana na ugunduzi wa hivi karibuni wa gesi, Twaweza na Benki ya Dunia walikusanya maoni ya wananchi kutoka Tanzania Bara. Takwimu zilikusanywa na Sauti za Wananchi, (www.twaweza.org /sauti) utafiti wa kwanza Afrika kwa njia ya simu mkononi wenye uwakilishi wa kitaifa. Matokeo kwenye muhtasari huu yametokana na takwimu kutoka kaya 1,562 zilizokusanywa katika awamu mbili za upigaji simu mwezi Oktoba/Novemba na Desemba 2013.

Matokeo muhimu ni:


- Asilimia 64 ya wananchi wa Tanzania wamesikia kuhusu ugunduzi wa gesi asilia, lakini karibu idadi hiyo hiyo wangependa kupewa taarifa zaidi.
- Watu walio wengi wana matumaini kuhusu matarajio ya gesi asilia, huku wananchi wanne kati ya watano wakiamini kuwa gesi asilia ni nzuri kwa ajili yao, watoto wao na nchi yao kwa ujumla.
- Watanzania asilimia 38 wangependa mapato yatolewe moja kwa moja kwa wananchi kama fedha taslimu wakati asilimia 43 wanafikiri kuwa mapato yanapaswa kwenda Serikalini ili yatumike kugharamia huduma za jamii kama vile elimu, afya na usalama.
- Robo ya Watanzania (26%) wanafikiri kuwa viongozi wa serikali watafaidika na mapato ya rasilimali, wananchi wengine (11%) wakiamini kuwa faida itaenda kwa matajiri.

## 2. Mambo nane kuhusu maoni ya wananchi juu ya rasilimali ya gesi asilia


### Jambo la 1: Wananchi wanafahamu kuhusu ugunduzi wa gesi lakini wangependa taarifa zaidi

Watanzania wawili kati ya watatu (64%) wanaonesha kuwa wamewahi kusikia kuhusu ugunduzi wa gesi, wengi wao wakiwa wamepata taarifa hizi katika kipindi cha mwaka uliopita (2013). Pamoja na hayo, Watanzania walio wengi wanahisi kuwa bado hawana taarifa za kutosha na ni Watanzania wawili kati ya watatu (65%, Kielelezo 1b) ambao wangependa kupatiwa taarifa zaidi. Wengi wao (60%) wanatarajia taarifa zitolewe na Serikali, au vyombo vya habari (26%).

**Kielezo cha 1a: Lini ulisikia kwa mara ya kwanza kuwa vitalu vya mafuta na gesi vimegundulika Mkoani Mtwara?**




**Kielezo cha 1b: Je, unafikiri kuna haja ya mtu fulani kukupatia taarifa zaidi kuhusu ugunduzi wa hivi karibuni wa mafuta na gesi nchini Tanzania?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi*, Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 2: Mtanzania mmoja kati ya watatu anaamini kuwa makampuni ya gesi tayari yanapata fedha kutokana na maliasili

Kukosekana kwa taarifa kunaweza kusababisha matarajio yasiyowezekana ifikapo kipindi cha kupata faida kutokana na gesi asilia. Utafutaji wa akiba ya gesi katika maeneo nje ya fukwe nchini Tanzania bado uko katika hatua zake za mwanzo na utachukua muda hadi kuanza kwa uzalishaji mkubwa, takriban miaka saba hadi kumi kulingana na makisio ya sasa.

Hata hivyo, wakati Watanzania asilimia 28 wanatambua kuwa itachukua kipindi kirefu kuanza kupata faida, asilimia 36 wanaamini kuwa makampuni tayari yameshaanza kupata faida, na Watanzania wengine asilimia 36 hawana uhakika juu ya jambo hili. Pengo hili la taarifa linapaswa kushughulikiwa kwa kuhakikisha mawasiliano ya wazi kuhusu matukio na mapato tarajiwa ya gesi yanapewa kwa wananchi. Zoezi hili litaepusha kutofautiana kwa matarajio ya wananchi ukilinganisha na hali halisi, ambapo hatimaye kungeweza kusababisha kutoridhishwa na usimamizi wa maliasili.

**Kielelezo 2: Je, unafikiri kuwa makampuni ya mafuta / gesi tayari yanapata fedha kutokana na ugunduzi wa mafuta na gesi bara na mkoani Mtwara?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 3: Watanzania walio wengi wana matumaini mema kuhusu manufaa tarajiwa ya gesi asilia

Ujumbe wa wazi kutoka kwenye utafiti wetu ni kuwa Watanzania wana matumaini na matarajio mema kuhusu maliasili iliyogunduliwa hivi karibuni nchini Tanzania. Kielelezo cha 3 kinaonesha kuwa Watanzania wanne kati ya watano wanaamini kuwa gesi asilia itakuwa yenye manufaa kwao, kwa watoto wao na nchi yao kwa ujumla.

**Kielelezo cha 3: Je, unafikiri athari za gesi asilia itakuwa nini?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 4: Watanzania wengi wana hofu kuwa faida ya rasilimali hii haitagawanywa kwa usawa

Tatizo linalojulikana sana kwenye sekta ya uvunaji wa maliasili ni kuwa faida haiwafikii wananchi, bali inahodhiwa na kundi dogo la watu, ambao wengi wao wanajihusisha na siasa au na viwanda.

Maoni ya Watanzania kwa kiasi fulani yamegawanyika juu ya suala hili: asilimia 31 wana matumaini kuwa faida itagawanywa kwa usawa kwa Watanzania, wakati asilimia 37 wanatarajia kuwa maafisa wa serikali au matajiri ndio wataofaidika zaidi na gesi asilia. Aidha, walipoulizwa waziwazi matatizo yanayohusiana na uchimbaji gesi asilia; asilimia 19 walisema kuhodhi kodi kwa makampuni ya kigeni, ikifuatiwa na kutokea kwa uhalifu / vurugu (11%), pamoja na rushwa ya viongozi wa serikali ikiwa imetajwa na wananchi (7%), wananchi walilitaja pia suala la "laana ya rasilimali" (haijaonyeshwa kwenye mchoro) kuwa ni moja ya athari.

**Kielelezo cha 4: Nani atanufaika na ugunduzi wa hivi karibuni wa gesi asilia nchini Tanzania?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 5: Watanzania wengi wanakubali gesi iuzwe nje ya nchi

Watanzania wengi hawana kipingamizi kuhusu uuzaji wa gesi asilia nje ya nchi. Kielelezo cha 5 kinaonesha kuwa Watanzania asilimia 61 wanasema uuzaji wa gesi nje ya nchi unakubalika ilimradi tu mapato yatumike kwa ajili ya maendeleo ya nchi. Hata hivyo, Watanzania watatu kati ya kumi (28%) wanafikiri kuwa gesi asilia iwe kwa ajili ya kuzalisha umeme na matumizi ya ndani ya nchi tu. Ni asilimia 5 ya Watanzania ndiyo wangependa gesi iuzwe nchi jirani za Afrika Mashariki tu.

**Kielelezo cha 5: Je, Tanzania iuze mafuta na gesi katika nchi nyingine ili kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 6: Watanzania wangependa makampuni ya ndani yashiriki katika sekta ya mafuta na ya gesi

Utafiti umebaibaini kuwa Watanzania wanaunga mkono wataalamu wa kigeni kusiadia katika uchimbaji wa gesi asilia. Watanzania zaidi ya nusu (52%) wanasema kuwa makampuni ya kigeni lazima yashirikiane na makampuni ya ndani (ambayo lazima yamiliki hisa yakama) wakati wa kuomba zabuni za vitalu vya mafuta/gesi. Theluthi moja ya Watanzania (35%) wanafikiri kuwa makampuni ya ndani yapewe kipaumbele kwenye zabuni.

**Kielelezo cha 6: Wakati wa kuomba zabuni za vitalu vya mafuta na gesi...**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 7: Wananchi wangependa kupewa mgawo wa mapato


Katika miaka ya hivi karibuni upelekaji wa moja kwa moja wa mapato ya fedha kutoka maliasili kwa wananchi umetajwa kuwa moja kati ya njia nzuri za kupambana na umaskini kwa ufanisi zaidi na kuongeza uwajibikaji kwa wafanya maamuzi na wanasiasa. Wakati jambo hili ni geni barani Afrika, utaratibu kama huo umeanzishwa kwenye baadhi ya nchi kama vile Alaska au Iran.

Sauti za Wananchi iliuliza swali lifuatalo: "Tanzania imekaribia kupokea fedha nyingi kutoka kwenye maliasili. Je, Serikali itumie fedha hizi kwa niaba ya Watanzania (kwa mfano, katika elimu, afya na usalama), au ipewe moja kwa moja kwa Watanzania kama fedha taslimu? "

Watanzania zaidi ya nusu (55%) wameunga mkono ugawaji wa mapato ya maliasili kwa niaba ya wananchi: asilimia 20 wangependelea fedha kupelekwa moja kwa moja kwa wananchi; asilimia 18 wangependa kuwe na mgawo sawa wa mapato kati ya serikali na wananchi, wakati asilimia 17 wangependelea Serikali ipokee asilimia kubwa ya mapato na wananchi wapewe kiasi kinachobaki.

Hata hivyo, kundi kubwa la Watanzania (43%) wangependa mapato yote yaende Serikalini (kwa ajili ya matumizi ya huduma za jamii kama vile elimu, afya na usalama).

**Kielelezo cha 7: Mapato ya mafuta na gesi yaende wapi?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

## Jambo la 8: Mapato ya gesi yatumike kwenye elimu na afya

Wananchi wangependelea mapato ya gesi na mafuta yasimamiwe na Serikali ili matumizi ya serikali kwenye huduma za jamii yaongezeke. Karibu nusu (46%) ya wananchi walisema kuwa matumizi ya mapato kwenye elimu na afya yatakuwa ni matumizi yenye manufaa zaidi ya mafuta na gesi, ikifuatiwa na matumizi kwenye miundombinu (20%) na matumizi ya mipango ya kupambana na umaskini (17%).

**Kielelezo cha 8: Ni matumizi gani ya fedha za gesi na mafuta kati ya yafuatayo yatayoleta manufaa zaidi kwa Watanzania?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa njia ya Simu za Mkononi – Awamu ya 9, Oktoba / Novemba 2013 na Awamu ya 11 Desemba 2013

# 3. Hitimisho

Wananchi walio wengi wana matumaini kuwa maliasili zitanufaisha familia zao, sasa na siku zijazo. Lakini wanafahamu pia matatizo yanayoweza kutokea. Baadhi wanahofia mapato yatokanayo na uchimbaji huu yatanufaisha makampuni ya kigeni, kuongeza migogoro, na rushwa kwa maafisa wa serikali.

Watanzania wengi wanaunga mkono ushiriki wa makampuni ya kigeni katika uchimbaji wa gesi. Hata hivyo, wananchi wangependa makampuni ya ndani kushiriki katika mchakato wa zabuni na kuwa na hisa nyingi zaidi katika ushirikiano wa kibiashara pamoja na makampuni ya kigeni.

Ili mrejesho kwa wananchi uwe na manufaa zaidi ni muhimu wananchi wapewe taarifa kamilifu. Kutaarifiwa na kupashana habari mara kwa mara, kwa uwazi, na kwa usahihi kuhusu uchimbaji wa gesi, uwekezaji na mapato yatokanayo na uchimbaji huu ni muhimu sana. Hii itahakikisha kuwa wananchi wanakuwa na matarajio halisi. Pia itatoa njia muhimu za kubadili matarajio hasi ya ‘laana ya rasilimali’ na kuwa baraka ya rasilimali.

Wakati wananchi wanaiamini Serikali kusimamia maliasili na kuwapa taarifa, wengi wangependa kupokea kiasi fulani cha fedha taslimu ili wagawane moja kwa moja mafao ya maliasili. Kwa sehemu, hii inaweza kutokana na imani kuwa watu walio serikalini na matajiri watanufaika zaidi na gesi. Hakika, maafisa wa serikali wataweza kusambaza taarifa kwa ufanisi na kusimamia rasilimali kwa maslahi ya wananchi wakati wao wenyewe wana shauku kubwa ya kuchuma mapato hayo? Majibu haya yanaibua swali linalofanana na hili: Je, wananchi wametaarifiwa kikamilifu kuhusu mwongozo na ulinzi dhidi ya vitendo viovu vinavyoweza kutokea?

Gesi ni hazina ya taifa ya utajiri ambao unapaswa kuzalisha faida kwa kipindi kirefu ikiwa hata baada ya kizazi cha sasa cha wanasiasa, watumishi umma na wataalamu kustaafu. Kutokana na hii, shauku iliyooneshwa na wananchi wa Tanzania kutaka mapato ya gesi yatumike kwa ajili ya uwekezaji kwenye mtaji watu (elimu, afya) kwa ajili ya vizazi vijavyo inapaswa kusikika na kuwekewa kipaumbele kwenye bajeti za kitaifa.